JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 20
***MISUNGWI***

Simu: 255-73298074
*BaruaPepe:ded@misungwidc.go.tz*
*Tovuti: www.misungwidc.go.*

Kumb. Na. MZA/MDC/S.10/35/VOL.I /9 11/07/2023.

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi anayofuraha kutangaza nafasi 3 za ajira ya kudumu kwa watanzania wote wenye nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na wenye sifa stahiki kuleta maombi kwa nafasi zilizoainishwa hapo chini baada ya kupata idhini ya kibali cha ajira chenye **Kumb Na. FA.170/359/01B/89** cha tarehe **31 Mei, 2023** kutoka kwa **Katibu Mkuu Utumishi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**. Mchanganuo wa nafasi hizo ni kama ifuatavyo:

### 1.0. DEREVA DARAJA II (NAFASI 01).

#### 1.1 Sifa za kitaaluma za mwombaji

(i) Awe Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(ii) Awe hajawahi kuajiriwa Serikalini.

(iii) Awe amehitimu na kufaulu kidato cha IV au VI

(iv) Awe na leseni daraja C1 au E ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

(v) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari **(Basic Driving Course)** yanayotolewa na chuo cha Ufundi Stadi (VETA) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(vi) Awe na namba ya utambulisho wa uraia (National Identification Number – NIDA).

**2.1. Kazi na Majukumu.**

(i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.

(ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.

(iii) Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari

(iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika.

(v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.

(vi) Kufanya usafi wa gari na

(vii) Kufanya kazi zingine kadri utakapopangiwa na mwajiri au msimamizi wako wa kazi.

**1.3. Ngazi ya Mshahara**

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara serikalini yaani TGS $B_1$.

**2.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III (VILLAGE EXCUTIVE –III) DARAJA III (NAFASI 02)**

**2.1. Sifa za kitaaluma za mwombaji:**

(i) Awe amehitimu na kufaulu Elimu ya kidato cha IV au VI

(ii) Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada / cheti cha Technician Certificate (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo:- **Utawala, Sheria, Usimamizi wa Rasilimali watu, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii** kutoka katika chuo cha serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**2.2. Kazi za kufanya /Majukumu**

(i) Atakuwa Mtendaji na mshauri wa Serikali ya kijiji na kamati zake katika mipango ya maendeleo.

(ii) Atakuwa Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya kijiji.

(iii) Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala Bora katika kijiji.

(iv) Atapaswa kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango na maendeleo ya kijiji.

(v) Atatafsiri sera, Taratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo za Halmashauri ya kijiji.

(vi) Atakuwa katibu wa kamati ya Halmashauri ya kijiji.

(vii) Ataongoza vikao vya maendeleo vya kijiji vitakavyowahusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.

(viii) Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umaskini.

(ix) Atakuwa kiongozi wa wakuu wa Idara na Vitengo wa kitaalamu katika kijiji.

**2.3 Ngazi ya Mshahara**

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara Serikalini yaani **TGS B1.**

**MASHARTI KWA UJUMLA.**

(i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka **45.**

(ii) Waombaji waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa

(iii) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi **(CV)** yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

(iv) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya elimu na Taaluma yaani nakala za vyeti vya kidato cha nne au sita, pamoja na vyeti vya taaluma **(professional certificate from respective board, Computer certificate) na picha 2 (passport size)** za rangi za hivi karibuni

(v) "Testimonials provisional result", "statement of result", hati ya matokeo ya kidato cha nne na kidato cha sita havitakubalika kabisa.

(vi) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (NECTA au NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatanishwe kwenye maombi.

(vii) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili tofauti na hapo ombi lako halitapokelewa.

(viii) Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe

(ix) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachuliwa hatua za kisheria.

(x) Waombaji watakao kidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili kwa namba za simu na anuani walizotumia kwenye barua ya maombi.

(xi) Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 25/07/2023 Saa 9.00 Mchana.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi,
S.L.P 20,
**MISUNGWI.**

**Tangazo hili limetolewa na**

Joseph C. Mafuru,

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MISUNGWI.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MISUNGWI

NB: ***Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na kwenye tovuti (website) ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ambayo ni** www.misungwidc.go.*